**HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA**

PROF.SARUNGI SEKONDARI,
S.L.P 02,
SHIRATI – RORYA,
0782052429 / 0756432603

**MZAZI / MLEZI WA ……………………………………..**

**MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE MWAKA 2024**

Nafurahi kukutaarifu kuwa uongozi wa shule pamoja na jumuiya nzima ya shule ya sekondari Prof. Philemon Sarungi wanakupa pongezi kwa mwanao kuchaguliwa kujiunga na shule hii kwa mwaka huu 2024. Shule itafunguliwa tarehe 08/01/2024 saa moja kamili asubuhi. Mwanao anatakiwa kufika shuleni kwa kuanza masomo rasmi bila kukosa.

**A. SARE YA SHULE (WAVULANA).**

- Wavulana wanatakiwa kuwa na suruali mbili (2) rangi nyeusi na rangi ya kijivu. Zisiwe za kununua sokoni na ziwe pana na sio za kubana.
- Mashati mawili meupe yenye mikono mifupi na lazima yawe mitumba au tomato
- Viatu vya ngozi vyeusi (soli fupi)
- Soksi nyeusi pea mbili na mkanda mweusi wa kuvalia suruali.

**B. SARE KWA WASICHANA**

- Wasichana watakuwa na sketi mbili (2) rangi nyeusi yenye rinda boksi kubwa mbele na nyuma.
- Sketi zote zinatakiwa kuwa ndefu zinazogusa kisigino.
- Mashati mawili meupe kama ya wavulana
- Vyatu vyeusi na soksi nyeupe.

**KWA WOTE WAVULANA NA WASICHANA**

- Counter books 10 (zote quire 4)
- Kalamu zake za kutumia
- Kamusi (dictaionary)moja
- T – shirt ya blue yenye kola iliyo na michirizi mieupe
- Masweta mawili ya dark blue na kijivu
- Rim paper double A moja kwa ajili ya mazoezi ya mara kwa mara.
- Siku ya kuripoti avae nguo za kijivu (suruali / sketi na sweta ya kijivu)

**VIFAA VYA USAFI**

- Wanafunzi wote wanatakiwa kuja na ndoo ya lita 10
- Wavula waje na mfagio wa chelae
- Wasichana mfagio mlaini wa ndani

## KIAMBATANISHO A

## SHERIA,KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

**A. MAMBO AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUFANYA**

1. Kutimiza wajibu wake kikamilifu na kwa ufanisi.
2. Kuhudhuria shuelni kila siku anayotakiwa kuwa shuleni.
3. Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.
4. Kulinda maadili yaliyomo katika kihimizo cha shule.
   **"ELIMU KWA MAISHA YAKO"**
5. Kuheshimu na kutunza kwa uangalifu mali ya umma.
6. Kushirikiana na kusaidiana na wenzake katika kazi.
7. Kuwa na utii na heshima kwa wanafunzi,wafanyakazi wote wa shule na raia wote kwa ujumla.
8. Kushiriki kikamilifu, kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote zinazotolewa na uongozi wa shule.
9. Kushiriki katika majukumu ya uongozi wa shule.
10. Kutii maagizo na kufuata maelekezo yote yanayotolewa na uongozi wa shule
11. Kufanya usafi binafsi wa mwili, mavazi na kutunza mazingira.
12. Kuwa mwaminifu.
13. Kushiriki katika michezo na shughuli za utamaduni wa Taifa.
14. Kusimama na kumsalimu mwalimu, mtu yeyote anayekuzidi umri anapopita.
15. Kutotumia lugha mbaya na matusi wakati wowote kwa wanafunzi wenzake,mwalimu na mtu yeyote.
16. Kuitika mara moja anapoitwa na kukimbilia aliko mkuu aliyemwita.
17. Kuheshimu Bendera ya Taifa,picha za viongozi wa serikali,Nembo ya taifa,wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
18. Kuheshimu ukumbi wa mikutano,mahali pa kulia na ofisi za shule.
19. Kusimama katika mstari wakati wote wa kupokea huduma.
20. Kuonyoosha mkono juu na kusimama wakati wa kuuliza na kujibu maswali.
21. Kukaa kimya wakati wote anapokuwa darasani ana atoke nje kwa ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyeoko.
22. Kuthamini na kutunza muda kazi zote zifanyike kwa kuzingatia ratiba iliyopangwa.
23. Kuwahi kwenye eneo la tukio anaposikia wito wa dharura
24. Kufika shuleni kwa tarehe zilizopangwa.
25. Kuwa ndani ya mipaka ya shule wakati wote akiwa shuleni.
26. Kutumia lugha ya Kiswahili na hasa kiingereza wakati wote mwanafunzi awapo shuleni.

**B. MAMBO AMBAYO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUFANYA**

i. Kuvuta sigara
ii. Kufuga ndevu
iii. Kufuga nywele ndefu zisizotunzwa katika hali ya usafi
iv. Kufuga kucha ndefu
v. Kuvaa mavazi yasiyo na heshima
vi. Kugombana
vii. Kuiga mitindo ya ki-huni mfa.kunyoa kipara
viii. Kujichubua ngozi ya mwili kwa kutumia madawa
ix. Kuja shuleni bila kuvaa sare rasmi ya shule.
x. Kuvaa kofia, bangili na mapambo mengine yoyote akiwa shuleni.
xi. Kutembea sehemu zifuatao isipokuwa kwa kibali maalum.
    (a) Chumba cha waalimu – staff room
    (b) Ofisi ya shule
    (c) Maabara
    (d) Jikoni
    (e) Nyumba za waalimu na wafanyakazi wasio waalimu
xii. Kutembelea sehemu zifuatazo;-
    (a) Vilabu vya pombe
    (b) Majumba ya starehe
    (c) Majumba ya kufikia wageni
xiii. Kuwa na simu, kamera na redio shuleni.

**C. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA.**

1. Wizi
2. Uasherati,ubakaji na ushoga
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
4. Uvutaji bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupiga au kupigana
7. Kuharibu kwa makusudi mali umma.
8. Kudharau Bendera ya Taifa
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
11. Kutoa mimba.
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza fujo au kuvuruga amani na usalama.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA

PROF.SARUNGI SEKONDARI,
S.L.P 02,
SHIRATI – RORYA.

**EXAMINATION MEDICAL FORM (HATI YA UTHIBITISHO WA TABIBU)**
Fomu hii ni muhimu kuleta shuleni ikiwa imejazwa kikamilifu siku ya kuripoti).

Ninathibitisha kwamba nimemchunguza mwanafunzi……………………………………..

1. Kinyesi ……………………………… Matokeo …………………………..
2. Mkojo ……………………………….. Matokeo …………………………..
3. Damu (Sickle cell/ B/S)……………… Matokeo …………………………..
4. Kifua kikuu (TB) …………………….. Matokeo ………………………….
5. Damu (Blood pressure – B/P)…………………. Matokeo………………….
6. Macho ………………………………… Matokeo………………………….
7. Ukoma (Athma)…………………… Matokeo…………………………..
8. Mimba kwa wasichana (Pregnancy) …………………. Matokeo …………

**USHAURI WA DAKTARI**

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………..

**……………………………..**
***TAREHE***

**……………………………..**
**SAHIHI NA MUHURI WA MGANGA**
**MKUU WA HOSPITALI YA SERIKALI**